

This booklet on Relationships with Men was developed by the Tanzania Home Economics Association with support from Our Bodies Ourselves. Other booklets and more information on the project are available at <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

MAHUSIANO NA WANAUME

Wale kati yetu tunaowategemea wanaume kwa mapenzi, urafiki, msaada, ngono au mchanganyiko wa mambo yoyote kati ya haya tunakumbana na maliwazo, furaha na malipo ya kipekee. Pia tunakabiliwa na changamoto na maswali ya kipekee ambayo hayana majibu rahisi. Ni kwa namna gani tunajadili kuhusu ngono salama na wapenzi wetu wa kiume? Tunajilindaje dhidi ya uonevu wakati tunajaribu kuwatambua wanaume wanaoweza kuwa wapenzi wetu? Tunawezaje kujenga mahusiano ya muda mrefu yanayoturidhisha na yenye usawa? Tunawezaje kujiendeleza sisi wenyewe na uwezo wetu, na wakati huohuo kuhakikisha tunadumisha hali ya kutegemeana na wapenzi wetu? Tunawezaje kuhakikisha usawa kati ya mahaba na malengo ya kielimu na/au kiamali? Tunalichukuliaje suala la kuwa bila mwenzi – namna linavyoweza kusababisha upweke, pamoja na kwa jinsi hali hii inavyoweza kutufanya turidhike – kadiri tunavyotazama nafasi kadhaa za kuweza kuwa na urafiki wa kimapenzi?

Kwenye dunia ambayo watu wamegawanywa sana na ujinsia, mahusiano tunayoyafanya na wanaume wakati mwingine huonekana kuwa na uthamani wa kipekee. Sura hii inalenga kujua ni kwa jinsi gani sisi kama wanawake tunaovutiwa na wanaume/na watu wa jinsia zote mbili, tunahusiana na wanaume ambao

tunaonyeshana au kufanya nao mapenzi, na kuanza nao maisha – na jinsi gani tunahusiana na nafsi zetu wenyewe katika mchakato huu mzima.

“MAMBO BINAFSI NI YA KISIASA” NA WIMBI LA AWAMU YA TATU YA HARAKATI ZA KUPIGANIA UKOMBOZI, HAKI, NA USAWA WA WANAWAKE

“Mambo binafsi ni ya kisiasa”, usemi uliofanywa maarufu na harakati hizi za wanawake, huelezea imani kuwa matatizo binafsi ya mtu ni dalili za matatizo makubwa zaidi ya kijamii. Wimbi la awamu ya pili ya harakati za kupigania ukombozi, haki, na usawa wanawake nchini Marekani lilitukia kwa wakati moja na kwa kiasi kikubwa kupewa mwongozo na kile kinachojulikana kama mapinduzi ya kijinsia ya miaka ya mwishoni mwa 1960 na 1970, ambayo yalipelekea suala la kujihusisha na mapenzi nje ye ndoa kuonekana kama kitu cha kawaida. Kama watetezi wengi wa nadharia ya haki na usawa wa wanawake walivyosisitizia kuwa ingawa mapinduzi haya ya kijinsia yangeweza kuwa changamoto kubwa kwa wanawake – hivyo kutuongezea tena tegemeo lingine la kijamii la kutimiza – yaliashiria mabadiliko chanya kwa afya ya wanawake kimapenzi, ikiwa ni pamoja na kupanuka kwa upatikanaji na machaguo ya uzazi wa majira, kuidhinishwa kisheria kwa utoaji wa mimba, na kuondolewa kwa adhabu za kimaadili dhidi ya ufanyaji mapenzi kabla au nje ya ndoa hatua kwa hatua.

Siku hizi, katika kile ambacho aghalabu huitwa wimbi la awamu ya tatu ya harakati za kupigania ukombozi, haki, na usawa wanawake, wanawake na

wasichana wanahamasishwa kwa mara nyingine tena kujua zaidi juu ya hisia za mapenzi na kuzielezea kwa namna ambazo kwa ujumla hazikuruhusiwa hapo awali, angalau kwa furaha mpya zaidi kuliko zamani. Lakini wimbi hili pia limetokea kwa wakati mmoja na utamaduni wenye nguvu unaokubalika na watu wengi ambao hutoa jumbe za juu juu tu kuhusu mapenzi na huchukulia kwa nadra mapenzi katika muktadha wa mahusiano ya kweli. Vipi kuhusu urafiki wa karibu sana na uwezekano wa kuweza kudhurika? Na vipi kuhusu haja ya kuhakikisha usawa katika amali na/au familia? Kwa namna gani mwanamke yoyote yule anaweza kupitia mandhari haya mapya – pamoja na sifa zake zote za kipekee za umbari, ukabila, umri, mtazamo wake kimapenzi, historia yake kijamii na kiuchumi, msimamo wake kisiasa, imani za dini, n.k. – bila ya yeye mwenyewe kupoteza msimamo wa “nafsi” yake au kutetereka, Au ni “nafsi”, angalau kwa kiasi fulani, ndio inatakiwa kupotea wakati anapokuwa kwenye mapenzi?

Huku suala la the “mambo binafsi ni ya kisiasa” likiwa kichwani, ni muhimu kukumbukuka kwamba kila wanaume na wanawake huingia kwenye mahusiano si tu tukiwa na historia zetu au “mizigo” bali pia na “uzito” wa matarajio ya vizazi kwa vizazi kutoka kwenye familia na tamaduni zetu. Ingawa maisha ya watu wa kawaida si rahisi sana ukilinganisha na aina fulani ya maisha ya kufikirika inayotamaniwa na wengi, wachache kati yetu tuna kinga dhidi ya aina hii ya maisha. Kwa bahati nzuri, wengi wetu – wanaume pamoja na wanawake – tunajitahidi kupingana na kuachana na matarajio haya. Ni kazi yenye changamoto, lakini pia inaweza kuwa ya kuisisimua,

hasa pale tunapopambana kwa pamoja na wanaume katika maisha yetu kutengeneza njia mpya za kuhusiana na kupendana.

KUWA BILA MWENZI

Iwe ni kwa kipindi kifupi tu kati ya uhusiano mmoja na mwingine au kama chaguo la maisha, kuwa pekee bila mwenzi kunaweza kuwa na faida nyingi na kumletea mtu furaha, licha ya kuwepo na jumbe zilizozeleka kwenye jamii kutoka katika familia na/au tamaduni zetu zinazokinza hili. Kulingana na vile tunavyoamua kufasili jambo hili, kuwa bila mwenzi kunaweza kumaanisha kuwa na mpenzi mmoja au wengi, kuwa na uhusiano wa kimapenzi wa muda mfupi tu, uhusiano wa kudumu bila ndoa, au kutokuwa kabisa na mahusiano ya kimapenzi au kimahaba.

“Nafurahia uhuru wa kuwa bila mwenzi, ambao kwangu humaanisha ninaweza kufanya miadi ya kimapenzi na wanaume lakini nisilale nao... Kutokuwa na jukumu la kuboresha nusu moja ya mahusiano kunamaanisha kuwa naweza kutumia muda huo kuwa na marafiki wengi zaidi, na muda mwingi zaidi wa kujifikiria – kuhusu mawazo na maswali yangu binafsi. Kwenye mahusiano, nimezoea kujiruhusu kuhusika na matatizo, mawazo, na masuala ya patna wangu, na huwa sijifikirii mimi mwenyewe sana. Ninapanga kutojikusisha na uhusiano mwingine wa muda mrefu. Ninafuhia aina ya maisha ninayoishi hivi sasa (ninao wanaume watano kwa sasa

ambao ninawasiliana nao kila baada ya muda fulani). Siku zote ninakuwa muwazi kwa wanaume ninaowekeana nao miadi. Kwa maneno mengine, ninawajulisha tangu mwanzoni kuwa sina mpango wa kujihusisha na mahusiano ya muda mrefu. Sitaki kumuumiza au kumpotosha mtu yeyote. Wanaume wengi hawajazoea mtazamo kama huu kutoka kwa wanawake, lakini wengi wao hawatatizwi sana na jambo hili. Nafhamu kuwa tabia hii itabidi ikome ikifika kipindi fulani, na bila shaka, kuna vipindi vya upweke vinavyoambatana na tabia hii. Kwa hiyo nini itakuwa suluhisho langu mwisho? Pengine muda utato jibu la swali hili.

Lakini pia kuwa wapweke bila wenzi kuna ugumu wake, hususan ikiwa tunahisi hatukuchagua kuwa wapweke, ila upweke ndio *umetuchagua* sisi, hasa tunapopitia vipindi vya ugonjwa, kiwewe, au kuondokewa na tumpendaye.

Nilibakwa takriban miaka mitatu hivi iliyopita, mara tu baada ya kumaliza chuo, na bado nasumbuliwa na jambo hili mpaka sasa. Nina mtandao mzuri wa marafiki na mtaalam wa tiba anayenisaidia kurudia hali yangu ya kawaida. Kitendo hicho kilifanywa na mtu ninayemfahamu. Kimeathiri sana uwezo wangu wa kuwaamini wanaume. Ninajua sitajihusisha na mwanaume yeyote kimapenzi kwa muda fulani. Ninahitaji muda ili kupata nafuu, na kufanya juhudi kusahau hisia nzito ambazo bado zinanisumbua, na kupata upendo kutoka kwa watu ambao ninajua hawataniumiza. Hii inajumuisha marafiki wa kiume pamoja na wa kike. Iko siku nitawekeana miadi na

mtu. Lakini kwa sasa ninafurahia kuwa peke yangu na mseja. Ila tu, bila shaka, katika zile nyakati ambapo ninajihisi mpweke kupita kiasi na kuanza kukilaumu kitendo kile cha ubakaji kwa kunisababishia hali hiyo kwa kiasi fulani. Hata hivyo, kwa ujumla, ninagundua baaadhi ya mambo yaliyo ndani yangu ambayo sikuwahi kudhani kama nilikuwa nayo.

Baadhi ya wanawake wanohitaji kupata watoto wa kuwazaa wenyewe lakini hawaoni wanaume sahihi wa kuwa baba wa watoto wao nao pia wanaongelea uchungu wa upweke kadiri umri unavyokwenda, licha ya ukweli kwamba wanawake wengi zaidi siku hizi tunaamua kuwa na watoto peke yetu. Mwanamke mmoja mwenye miaka thelathini na tano anasimulia:

Miaka michache iliyopita, baada ya kuvunjika kwa uhusiano kulikonipa uchungu mkubwa, nilipiga mahesabu mengi sana kwa wakati mmoja: itanigharimu kiasi gani – kifedha na namna nitakavyojitolea kimaisha: kulea mtoto peke yangu? Kupanga mtoto? Kujaribu mtoto wa kupandikiza? Niliwaelezea wazazi wangu juu ya jambo hili... nilipata misaada mkubwa wa kimawazo. Mwishowe niliamua kuwa haukuwa muda muafaka. Ninahitaji msingi imara kifedha na kitaaluma kumpa maisha mazuri mtoto. Kulifikiria suala hili kwa makini kulinisaidia kupunguza unyonge na kuniongezea uwezo wa kufanya maamuzi ya kujihami. Niliweza kukabidiliana na suala hilo. Kwa sasa nafahamu kuwa kunaweza kuwepo na machaguo mengine

mbadala mbeleni kuliko nilivyokuwa nafikiria hapo awali. Kuwa mpweke hakuogopeshi sana tena.

Wale kati yetu ambao ni wazazi tusio na wenza – iwe kwa kuamua au kutokana na sababu mbalimbali – tunakabiliwa na seti ya changamoto na tuzo ya kipekee. Mtaalam wa matibabu ya kisaikolojia mwenye umri wa miaka thelathini na saba ambaye pia ni mama wa wavulana wawili aliyeachika anasema linapokuja suala la kulea watoto mwenyewe, ‘kitu cha muhimu zaidi ni kuwa na mfumo imara wa kukupatia msaada.’ anaendelea:

Hivi karibuni nimesoma juu ya kinamama wasio na wenzi wanachangia nyumba na watoto wao; Hili linaonekana kama wazo zuri linaloweza kufanyiwa kazi. Nadhani bado ninaamini kuwa liinapokuja suala la kulea watoto, “kinahitajika kijiji.”

Ingawa jamii nyingi hupenda wanawake wasio na wenza wanojitegemea, wengi wetu tumeambiwa tokea utotoni kuwa maisha yetu hayatakuwa kamili mpaka pale tutakapopata mwanaume. Ugumu hasa wa kuwa bila mwenzi, wanawake wakati mwingine husema, sio upweke bali ni mitazamo hasi ya kijamii kutoka kwa watu wengine inayotubidi tukabiliane na, imefikia kiasi kwamba tumeshaichukulia mitazamo hii kuwa kitu cha kawaida.

“Nina miaka 30, na sijaolewa. Nimedokezwa na watu kuwa wanadhani mimi siwajibiki, au kuwa lazima nitakuwa mwanamke mkoo. Pale wazazi wangu na watu

kazini wanaponiuliza tena na tena ikiwa “nimeshakutana na mtu,” huwa nageuza jambo hili kuwa utani, lakini moyoni nafikiria, “Ninafuraha kadiri ninavyoweza hivi sasa, na huwezi kulielewa hili.”

Wengi wetu tulifundishwa tangu tukiwa na umri mdogo kabisa – moja kwa moja au kwa namna isiyo wazi sana, kupitia nguvu za kifamilia au za kiutamaduni – kutafuta mwanamume mwenye sifa za kuweza kutoa msaada na tujishikize kwake. Kwa njia hii, tutaweza kuwa wakamilifu. Wasichana wengi huanza kukabiliana na changamoto hii wakiwa sekondari, kama sio kabla ya hapo, na kuona hali hii ikizidi kukua wanapoingia high school.

Nilivyokuwa nakua, hususan wakati nipo sekondari na chuoni kulikuwa na shinikizo kubwa la kijamii na kitamaduni la kutafuta mwenzi na kuwa msichana wa jamaa fulani. Marafiki zangu wakubwa wa kike hapo chuoni hatimaye wakawa na maboifrendi, na walitumia muda wao wote wakijaribu kuwafurahisha na kuwafahamu zaidi badala ya kujifahamu sisi wenyewe. Mara kwa mara nilihisi msukumo kutoka kwa kila mtu anayenizunguka kutafuta “mtu wa kunimiliki”, lakini mimi nilitaka kuwa mtu wangu mwenyewe, bila msukumo kutoka kwa mtu mwingine. Nina miaka 27 na bado ni mwanamke mseja, mwenye malengo makubwa, na ninafurahia sana kwa kuwa sikuwatafuta mwenzi wakati marafiki zangu wote wanafanya hivyo. Hakuna tatizo lolote ikiwa mtu utaolewa na kupata watoto, lakini lisiwe jambo la kukimbilia pale unapokuwa mpweke au unapokuwa haujui kitu

kingine cha kufanya. Nisingekuwa nimefanya hata nusu ya mambo niliyoyafanikisha mpaka sasa, au kuona yale niliyoyashuhudia, au kuandika au wala hata kufikiria kuhusu mawazo yangu mwenyewe endapo nisingeamua kuwa mseja. Na kuna wanawake waseja kama mimi wengi tu kila mahali, bila wenzi na wanafurahia hali hiyo.

Wanawake wengi waseja pia wanasisitizia umuhimu wa kuwa shupavu vya kutosha ili kuweza kufahamu ni kwa namna gani na kwa wakati upi, kama itabidi, kuendelea na maisha yako – iwe katika kukuza zaidi mahusiano ya kimapenzi au katika kuanzisha mahusiano mapya.

Nilipoachana na mpenzi wangu, nilikuwa na bahati ya kuwa na marafiki wachangamfu na wenye upendo ambao walinikumbatia na kuniliwaza. Lakini bado nahisi kukosa ule mgusano wa kimahaba wa mwili mzima. Sikutaka kuharakisha kujiingiza katika mahusiano mapya kwa sababu tu nilikuwa na hasira sana kiasi kwamba sikutaka hata kuguswa. Moja ya suluhisho ilikuwa ni kupata msingo kila baada ya wiki kwa miezi kadhaa.

Idadi ya wanawake wanakutana na wanaume kupitia huduma za kuweka miadi kwenye mtandao inazidi kuongezeka. (Kwa maelezo zaidi, tazama “Miadi ya haraka haraka na kwenye Mtandao [W26] kwenye tovuti, www.ourbodiesourselves.org.)

Tunapokuwa kuwa imara na wenye furaha sisi wenyewe, tunakuwa kwenye nafasi nzuri ya kuweza kuchagua kwa uhuru na kwa umakini wanaume tunaokuwa nao

Mahusiano Na Wanaume (“Relationships with Men”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

karibu. Kuanzisha uhusiano salama na wenye usawa na mwanaume kunaweza kuwa changamoto tunayoitafula na kuifurahia kutokana na mvuto, mahaba na mapenzi kutoka pande zote mbili.

UWEZO BINAFSI NA MAHUSIANO

Kwangu mimi, uwezo binafsi wa mtu dhidi ya mahusiano na wanaume humaanisha kuwa karibu na kile ninachokitaka na kukihitaji na kumwelezea mahitaji haya na mwenzi wangu moja kwa moja. Kivitendo, hii inaweza kuwa ni mchakato wenye changamoto kubwa – kuwa karibu na kile kitu ambacho mtu anakitaka ni suala la linaloweza kuchukua muda mrefu sana kulitekeleza. Kumwelezea mwenzi wako moja kwa moja suala hili sio kitu rahisi. Nadhani wanawake wamewekea umakini sana kwenye vitu ambavyo watu wengine wanavitaka na kuvihitaji kiasi kwamba tupoteza mawasiliano na mahitaji na matamano yetu ya ndani! Kwa upande mwingine, wanaume wamezidisha mawasiliano na vile vitu wanavyovihitaji hasa na wanaufahamu kidogo zaidi juu ya kuwahudumia wengine.

Uwezo wa binafsi una maana mbalimbali kwa watu tofauti: kujiona, kutambulika (kama mtu binafsi au kama sehemu ya kundi), kujivunia umbile la mwili, kujiamini, kufurahia kitu mtu anachofanya, hali ya kujiona kutoa mchango kwenye jamii, uwezo mzuri kifedha/kimapato, kujitegemea, uwezo wa kuwasiliana... na listi inaendelea.

Kwa wengi wetu, kutafuta uwezo binafsi kunamaanisha kutafuta nguvu ya ndani – hali ya kuwa “sisi wenyewe” na kujitambua, nini tunahitaji na nini tunataka.

Kwangu mimi, mwonekano wa mwili wangu ni suala la muhimu katika vile ninavyojisikia; ni sehemu ya kujistahi. Mazoezi ya mwili (kwa upande wangu, kukimbia mara kwa mara) yananisaidia nijisikie mkakamavu kimwili na nichangamke kiakili, jambo linaloathiri utayari na uwezo wangu wa kuwa na uhusiano karibu na mtu. Ninaamini kuwa kama mtu atakuwa na imani thabiti kwa nafsi yako mwenyewe, itakuwa ni jambo rahisi sana kwake kuwa na uhusiano na mtu mwingine. Hii inamaanisha kuwa na msimamo na mwenye kujiamini wakati wa kujieleza, kuwa shupavu katika kukabiliana na changamoto za maisha (kimwili na kihisia), kujua naungwa mkono na watu wanaonizunguka, na kutumia muda wa kutosha kwenye vitu navyofanya nje ya mahusiano (kazi, marafiki, n.k.).

Mambo ya kijamii na kitamaduni yanaweza kubadilisha kwa kiasi kikubwa namna mtu anavyojielewa akiwa ndani ya mahusiano. Kila mwanamke anakabiliwa na seti ya kipekee ya machaguo na changamoto ambayo inamwezesha na kumwamisha katika mambo fulani.

Mwanamke mwenye umri wa miaka thelathini na tano aliyekulia Japani na anayeishi Marekani kwa sasa anasema:

Mara kwa mara nimejikuta nikijaribu kujilinda dhidi ya taswira ya wanawake wa Kiasia ambao hukubali kila jambo bila kupinga, wasioonyesha hisia kwa urahisi...na

matokeo yake, nimekuwa nikifanya mambo kinyume kabisa ili kuonyesha kuwa mimi sina mtazamo kama wanawake wengine wa Kiasia. Niko makini sana na wanaume wanaofahamu utamaduni wa kiasia, hasa wale ambao wamedekezwa na ukweli huu kwa sababu tu ni wazungu (au Wamarekani)... Kwangu mimi, kujistahi ni suala la muhimu. Kuwa mtu wa chini...na kupambana na mtazamo uliozoeleka na wengi kwenye jamii (ambao ninaweza kuwa naufikiria kichwani mwangu) kunapunguza uwezekano wa mimi kuwa kama mimi. Ingawa napenda jinsi rafiki yangu wa kiume anavyoeshimu maamuzi yangu, mara nyingi najikuta nikimtegemea afanye mambo kiume zaidi na kwa kunihami.

Pamoja na kuzungukwa na mambo binafsi, na bado tena kuna masuala ya kijamii, kitamaduni, kiuchumi na kihistoria ambayo kwa pamoja yanachangia kuumba tabia ya mtu huyu. Watetezi wa nadharia ya haki na usawa wa wanawake wamesisitizia kwa muda mrefu kuwa kupata madaraka na baadhi ya matendo kwenye jamii vina uhusiano wa karibu na uwezo binafsi wa mtu na namna anavyojistahi – na kwa maana hiyo – vitendo vya kimapenzi – kwenye maisha binafsi.

Wanawake wanaobaguliwa kwa sababu ya ulemavu wao, kwa mfano, hupambana na masuala kibao ya kibinafsi na kijamii ambayo hayawakabili wanawake wasio na matatizo yoyote ya kimwili. Mwanamke mmoja aliye kwenye miaka ya arobaini hivi ambaye alizaliwa na matatizo makubwa ya misuli kwa sababu ya matatizo aliyoyapata mama yake ambaye ni mzawa wa Marekani anayeishi maeneo ya kijijini

wakati akijifungua, sasa anatumia baiskeli maalumu aliyotengenezewa kwenda kazini kila siku. Licha ya kwamba alikaa nyumbani muda mrefu kuliko ilivyo kwa wanawake wengine wengi, mara alipoanza kujitegemea na kushikilia wadhifa mzuri (akiwa kama mkurugenzi wa programu ya kuishi kwa kujitegemea iliyo mahsusi kwa Wamarekani Wazawa), aliweza kuanzisha mahusiano ya kiutu uzima zaidi na wanaume:

Siku zote nimekuwa nikiwafahamu watu wengi kupitia mahusiano ya kifamilia na kikabila, na siku zote nimekuwa mtu wa kutoka mara kwa mara. We! najua kuchekesha watu. Lakini mpaka pale nilipofahamu kuwa naweza kufanya hivi peke yangu, mara nyingi nilikuwa najisikia kukata tamaa na kuishiwa nguvu. Niliishi na wazazi wangu. Sikufanya kazi. Niliulaumu ulimwengu. Kuna wakati nilijilaumu mwenyewe. Nikiwa kama mwanajumuiya wa taifa la Omaha, siku zote nilikuwa mtu shupavu ambaye nilikuwa na mtazamo imara wa kiroho: kuheshimu maisha, uhusiano kati ya viumbe hai vyote, na mawazo ya aina hii. Mambo haya yalinisaidia sana. Pia, pale nilipoanza kuishi peke yangu na kupata imani zaidi ya kufanya hivyo...na nilipoanza kukutana na watu wengi zaidi kupitia kazi nayofanya na safari zangu, kuanza kupata heshima kutoka kwao – nilianza kujiheshimu zaidi pia. Nilianza kujenga mahusiano ya karibu zaidi na watu – ikiwa ni pamoja na wanaume - nje ya familia na kabila langu. Niliona mabadiliko fulani....Nilianza kujisikia kama nina kitu cha kipekee cha kutoa kwa watu. Bila shaka siku zote nilikuwa nacho; Kweli nilikuwa nacho lakini sikuwa naelewa.

Ubaguzi wa rangi na kitabaka unaweza pia kuathiri uwezo wa wanawake katika mambo binafsi na ya kijamii. Kwa upande mwingine kabisa, mashinikizo waliyonayo wanawake ya “kuwa na kila kitu” yanaweza kudhoofisha ile hali ya uwezo binafsi wa mtu kwa kusababisha kiwewe cha ndani kwa ndani, kama sio kukata tamaa kabisa. Mwanasheria mmoja mchanga anasema:

Nadhani ile fikra ya “mwanamke mwenye uwezo wa kufanya kila kitu” inawaharibu wanawake. Ninao marafiki wengi wanawake wenye taaluma zao, lakini baado wengi wetu tunataka kuolewa na kupata watoto. Tunategemea kujiendeleza na taaluma zetu na kuwa na majukumu sawa ya nyumbani/kulea watoto. Hata hivyo kiukweli binafsi sifahamu jambo hili linavyoweza kutokea. Maeneo yetu ya kazi bado yametawaliwa na mawazo kuwa wafanyakazi (wanaume) wana wenzi wao (wanawake) majumbani ambao wana jukumu la kushughulikia masuala yote ya nyumbani na kuwaacha wanaume washughulike tu na kazi...aina hii ya maisha sio nzuri kwa wanaume, wanawake au familia. Badala ya kuendelea kudhani kuwa mwanamke anaweza “kuwa na kila kitu” lingekuwa suala la maana zaidi kuboresha maeneo ya kazi ili kwamba wote, wanaume na wanawake, waweze kuwa na maisha bora wao pamoja na familia na marafiki zao.

Mahitaji ya kiuchumi yatatupa mzigo mkubwa sana. Kwa kuwa miili yetu inaweza kuchoshwa na kazi, umasikini au ugonjwa, vile vile inaweza kuchangamshwa kupitia kazi au shughuli tofauti nje ya kazi, ili kupata uwezo, nguvu na afya zaidi. Kwa wale baadhi yetu ambao tumejaribu kujipima uwezo wetu dhidi ya wanaume na kujikuta

Mahusiano Na Wanaume (“Relationships with Men”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

tunapungukiwa tumekuwa tukijaribu kukuza viwango vinavyolingana vya nguvu za mwili na uwezo wa kutetea maslahi yetu.

Moja kati ya vitu nilivyojitosa kufanya katika wa umri wa miaka 54 ilikuwa ni kufanya mazoezi ya judo [mchezo wa sanaa ya kujilinda wa Kikorea]. Siku zote nimekuwa nikivutiwa sana na michezo wa sanaa za kujilinda lakini kamwe sikuthubutu kujaribu kuifanya. Nilikuwa najaribu kubadilisha mtazamo wangu wa muda mrefu; kufanya angalau kitu kimoja kinyume na desturi yangu haitokuwa vibaya, nilijiambia. Katika kipindi chote cha ndoa, sikuwahi hata siku moja kubishana na mume wangu, na nikaona kuchukua mazoezi haya labda kungeweza kunisaidia zaidi kutetea maslahi yangu. Mume wangu hakupendezwa kabisa na kitendo “cha kiume” kama kile. Lakini sikubadilisha mawazo.

Baadhi yetu tunaona kwamba kufanya aina fulani ya matendo – kama vile kusali, kutaamuli, kuandika, matembezi, kucheza au kusikiliza muziki – pia kunatupatia chanzo cha nguvu ambacho tunaweza kukitegemea katika kuhakikisha mahusiano yetu hayavunjiki.

Kwa upande mwingine, baadhi ya wanawake ambao wameshajijengea uwezo wao binafsi kwa kiasi kikubwa – iwe uwezo huu unatokana na mafanikio kifedha, nguvu za mwili au la – hugundua kuwa wanaume huogopeshwa na mafanikio yetu na jinsi tunavyojiamini.

Nimeshawahi kuwa na wanaume wengi ambao mara ngingi waliogopeshwa na kazi yangu, uwezo wangu kifedha na namna ninavyojiamini. Ninashughulikia mwenyewe gari langu, nakarabati taa zangu mwenyewe, nasafiri pekee yangu. Nimekuwa naambiwa kuwa siwafanyi wanaume wajisikie kama wanahitajika katika maisha yangu. Nadhani hili limenipunguzia sana machaguo yangu ya kuweka miadi ya kimapenzi na wanaume. Nimeamua kuwa pekee yangu kuliko kufanya kinyume na msimamo wangu.

UHUSIANO WA KARIBU SANA: KUFHAMU BAADHI YA VIKWAZO

Fikra yangu ya mwanaume aliekamilika itakuwa ni mwanamke kunaswa na umbile la mwili wa kuvutia wa mwanaume. Kwa namna hii nitaweza kupata hisia na uangalifu ninaoutafuta, pamoja na makalio mazuri na mabega mapana.

“Tunaposema urafiki wa karibu sana tunamaanisha nini? kwa nini sote tunautamani sana, na ni kitu gani hasa tunachokitamani? Ukaribu wa kimwili? Rafiki wa karibu tunayeshirikiana kila kitu? Kukubaliwa jumla bila sharti lolote? Masharti yaliyo wazi ambayo tunaweza kuchagua? Au mchanganyiko wa yote haya? Je yote haya yanaweza kutoka kwa mtu mmoja pekee? Yana mwisho? Tunaupataje? Na, tunawezaje kuuendeleza?”

Kwangu mimi, uhusiano wa karibu sana ni ile hali ya kipekee ya uhusiano ambapo tunajisikia salama vya kutosha kuweza kujiweka wazi kwa kila kitu na bado

Mahusiano Na Wanaume (“Relationships with Men”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

tukafahamu kuwa tutaendelea kupendwa. Changamoto kubwa kwenye mahusiano ya aina hii ni kwamba iie tuweze kuyafanikisha, ni lazima tujiweke katika hali ya kuwa tayari kwa chochote, hasa kukataliwa. Lakini mahusiano ya aina hii hutupatia usalama wa kuwa wenye upendo zaidi kwa wenzi wetu na hata kujipenda zaidi wenyewe pia...

Vikwazo ambavyo nimevipitia katika suala zima la kuwa uhusiano wa karibu na wanaume ni pamoja na hofu zangu mwenyewe za kuwa na mapungufu, kuwa na mwenzi ambaye hapendi sana kuwasiliana (na fikra zangu kama vile “siko kichwani mwake”), na mwenzi wangu kuvunja uaminifu hivyo kunifanya nisijisikie salama au kutopendwa.

Urafiki wa aina hii huhitaji uwazi. Hii inamaanisha kuwa na moyo wa kushirikishana mahitaji, matatizo au katika kipindi kigumu kihisia; hata ikiwa tunaogopa mambo haya yanaweza kuwafanya wenzi wetu watukimbie. Kusita kuwa wawazi kwa hofu kuwa tutawaumiza wengine, siku zote huleta matokeo kinyume na tunavyotarajia. Tunajihadaa sisi wenyewe na kujikosesha nafasi ya kuunganika zaidi na wenzi wetu, na vile vile tunawanyima wapenzi wetu nafasi ya kutujua kiundani, na kutufanyia matendo yanayotokana na mapenzi ya kweli hasa.

Kwa kuwa hofu hongeza hofu zaidi, mashaka nayo huzaa mashaka zaidi. Basi kumbe kutokuwa na mashaka kunaweza pia kutokana na hisia kuwa wenzi wetu hawana mashaka yoyoye na vile jinsi walivyo – salama vya kutosha kiasi kwamba

hawaogopeshwi na uwezo tulionao au mahitaji yetu, wala na hisia za watu wengine, zao au zetu za kimapenzi.

Kwangu mimi, vikwazo vikubwa kwa uhusiano wa karibu na wanaume walio wawazi ni tabia yao ya mara kwa mara kuchukia wapenzi wa jinsia moja. Kijana mmoja muwazi mwenye mtazamo usiopendeza dhidi ya majamaa wawili walio kwenye uhusiano wa kimapenzi siku zote ameonekana kubadilika pia kuwa kijana muwazi mwenye matatizo ya kuafiki kuwa wanawake ni watu wanaoweza kuwa na usawa na wanaume. Kwa kuwa uhusino wa aina hii unahitaji uaminifu, kwa kuwa nadhani inahitajika kuwa mtu unayejiamini kuweza kumuamini mtu mwingine, wanaume ambao wana mashaka juu ya ujinsia wao kwa kuwa kuna wanaume wanafanya mahusiano na wanaume wenzao, kwa mtazamo wangu, hawawezi kuwa na aina hii ya uhusiano tunaouzungumzia, na mwanamke muwazi anabidi kuwaepuka.

Zaidi ya hapo, tofauti za kitamaduni zinaweza kuleta changamoto mbalimbali kwenye mahusiano ya karibu ya kimapenzi. Kijana mmoja wa Kiajentina mwenye umri wa miaka ishirini na mbili aliyehamia Marekani anasema kwamba, changamoto kubwa kuliko zote katika kufanya mauhusiano ya karibu na wanaume imekuwa ni kuwaingiza wanaume wa Kimarekani kwenye familia yake:

Ilikuwa vigumu sana kwao kuuelewa uhusiano wa karibu uliopo kati yangu na mama yangu. Kumuelezea mama yangu baadhi ya siri zangu na kushirikishana naye baadhi vitu hayakuwa ni mambo ambayo wanaume hawa waliyaelewa au hata

kuyapenda sana. haikuwa rahisi kwa mimi kumkubali kijana yoyote bila ridhaa au maoni ya mama yangu. Suala lingine lilikuwa ni kufanya mapenzi. Sikuwa tayari kufanya mapenzi na mtu nisiye mpenda...Wavulana wengi walitaka tufanye mapenzi mara tulipokutana kwenye miadi ya mapenzi kwa mara pili. Wengi wao waliogopa kufahamu kuwa nilikuwa bado bikira katika umri wa miaka 19. Ni mtu mwenye uelewa mkubwa na mwenye kutaka kufahamu uhusiano uliokuwepo kati yangu na familia yangu kuweza kuishinda hofu ya ushawishi mkubwa wa wazazi wangu kwangu na kuheshimu ubikira wangu... hata hivyo, japo kuwa nilikuwa nimelelewa kwenye mazingira yanayodumisha utamaduni, ilinibidi kupindisha na kutofuata baadhi ya sheria na kanuni kutoka nchini kwetu ili niweze kuwa na uhusiano mzuri na mwenzi wangu.

Dhana yetu ya uhusiano wa karibu sana – na kile tunachokitaka kutoka kwa rafiki wa karibu sana – inaweza pia kubadilika baada ya miaka kadhaa na kadiri sisi na mahusiano yetu tunavyokua. Baada ya miaka kumi na minne ya ndoa na Mmarekani mwenye asili ya Kichina – mhitimu mmoja wa miaka thelathini na sita, Mkatoliki, mwenye asili ya Kimexico na mama wa wavulana wadogo wawili anafasili urafiki wa karibu kama “ni mkutaniko wa mawazo”:

Au ni kwa sababu hili huhusu kila kitu wanachokutana nacho watoto wetu siku hizi katika vitanda vyetu, makochi yetu, mezani, na kwenye magari? Ukaribu umekuwa kitu kilichonyakuliwa kutoka pembezoni mwa maisha yetu yanayozunguka uleaji wa

watoto. Hapo kabla, ilikuwa ni kujikunyata kwenye kochi. Hapo mwanzoni kochi lilikuwa kama kipimo. Sasa hivi limekuwa ni sehemu ya kujibwaga mwisho wa siku tunaporudi na uchovu wetu, au labda sehemu ya kuangalizia filamu. Hata hivyo, je naweza kukuambia kitu gani natamani sana kaika hatua hii ya uhusiano wetu? Kutembea mrefu katika ufukwe wa bahari unaovutia...peke yangu. Nautamani sana ukaribu na nafsi yangu MWENYEWE...Nadhani pia uhusiano wa aina hii ni kitu kinachoundwa panapokuwa na nafasi ya kufanya uaminifu wa kutosha. Nafahamu kuwa ninaweza kuwa mimi kama mimi – na mambo yangu mazuri, mabaya na yasiyopendeza – na ndani ya kikomo cha akili timamu, [mume wangu] atakuwa bado ananipenda. Ninatumia muda mwingi sana katika maisha yangu nikijaribu kuthibitisha uwezo wangu kwa watu wengine: Kamati ya tasnifu yangu, watu tofauti naokuwa nao kwenye warsha mbalimbali, usaili wa kazi, na bado tena na wazazi wangu! Hata na watu mtaani: Je, ninapokuwa mbele ya jamii ninajichukulia kama mama “mzuri”, mwanamke anayevutia, au mtu stahifu? Pengine [mume wangu] ndiye pekee tu maishani mwangu ambaye “sitendi” vitu kwa ajili yake.

Mwanamke mmoja aliye kwenye miaka ya thelathini ambaye anajiona kuwa huntha anaongelea juu ya uhusiano wake wa kwanza:

Mimi na mpenzi wangu wa kwanza wote hatukuwa na uzoefu wowote ule, lakini tulikuwa marafiki wakubwa pia, hivyo tulishirikishana uaminifu na uwazi – utayari wa kujifunza, kujaribisha, kutaniana, na kimsingi hatukuuchukulia uhusiano wetu kwa

umakini sana. Hivyo hata baada ya kuwa tumeshakuwa wakubwa na tumekuwa watu tofauti kabisa kwa sasa, bado kuna vitu dhahiri ambavyo bado tunashirikishana.

Ni suala linalohitaji jitahada kubwa, hasa kadiri umri wangu unavyozidi kwenda, kuwa na uwazi kama huu wa bila kujali kitu katika uhusiano wa kimapenzi. Watu wanaonekana kuwa wastahimilivu na dhaifu zaidi kulingana na umri wao, lakini wapenzi niliowapata na ambao wanaweza kuwa hivi – wawazi na wenye utani – ndio ambao bado nawafahamu na kuwategemea, na kiukweli, ndio ambao bado nawapenda.

KUWA SALAMA

Wanawake waseja tunakabiliana na vizingiti vya kipekee kadiri tunapoanza mahusiano mapya na wanaume. Yafuatayo ni baadhi ya mambo yanayoweza kukusaidia kubaki salama:-

- Ikiwa unaweka miadi ya kimapenzi na mwanamume, chukua namba yake ya simu na si wewe umpe yako. Kutana naye sehemu ya umma yenye watu wengi. Mtaarifu rafiki yako utakuwa wapi na utampigia asubuhi inayofuata kumjulisha kuwa ulirudi salama. Epuka kutumia dawa au pombe nyingi siku ya kwanza kukutanaye kwenye miadi.
- Endapo unakutana na mwanamume usiyemfahamu, kuwa makini na maeneo yanayokuzunguka na chungu kinywaji chako. Matapeli wa mapenzi wanajulikana kwa tabia yao ya kuwawekea watu dawa za kulevya kwenye vinywaji zinazosababisha kupoteza kumbukumbu kwa muda mfupi. Kaa ukifahamu kuwa unajiweka katika hatari kubwa kwa kumpeleka nyumbani kwako mtu ambaye ndio kwanza umekutana naye.
- Kuwa tayari kujadili kuhusu na kufanya ngono salama na mwenzi wa kiume. Fahamu juu ya tahadhari za kuchukua dhidi ya magonjwa ya zinaa, ikiwa ni pamoja na ukimwi

(tazama Sura ya 14, “Ngoni Salama”) na kuhusu uzazi wa mpango (tazama Sura ya 18, “Uzazi wa Mpango”). Kama unadhani mnaweza kujamiiana, hakikisha umeandaa kinga. Usidhanie kuwa endapo mwenzi wako atakuingilia bila kinga, inamaanisha anakujali sana ndio maana ameshapima tayari. Wanawake wengi wasiokuwa na ukimwi/magonjwa ya zinaa mara nyingi wamekuwa wakiwa na fikra kama hii lakini wakaishia kuvunjika mioyo – kama sio kuambukizwa - baada ya kugundua mambo ni kinyume na walivyodhani.

- Jifunze kwanza aina zote ngono yenye kuburudisha na kuridhisha unazoweza kufanya huku ukiwa umelinda afya yako (tazama Sura ya 12, Hisia za Mapenzi). Hii inamaanisha majadiliano mtakayoyafanya sio lazima yawe juu ya mambo ambayo *hauwezi* kuyafanya.
- Jua sheria zako mwenyewe. Kila mwanamke ambaye anajamiiana mara kwa mara hufanya machaguo juu ya aina zipi za hatari yuko au hayuko tayari kukabiliiana nazo. Fahamu mipaka na mahitaji yako ya kujilinda kabla hujaingia kwenye hali ya kuweza kufanya mapenzi, wakati ambao uwezo wako wa kufanya maamuzi unakuwa mdogo.

KUHOFIA MAHUSIANO YA KARIBU SANA

Kuvuka kuingia uwanda mpya wa mahusiano ya karibu kimwili na/au kihisia kunaambatana na hatari zake. Tunaweza kuwa na hofu kwamba tutashindwa kuafikiana na wenzi wetu, au kwamba endapo tutajaribu kufanya hivyo wenyewe tunaweza kujikuta tunaumia kimwili, kihisia, au hata kisaikolojia. Au tunaweza kuogopa kuwa tunaweza kukataliwa kwa sababu “hatujakamilika.”

Lakini bado hofu ni silika asilia, hali ya kawaida inayotokea panapokuwa na au panapokuwa na uwezekano wa kutokea hatari. Mbinu ya kwanza kuelewa hofu ni kuitambua. Hapo ndipo tutakapojua wapi na wakati gani ni muafaka, na hapo tu

ndipo tutaweza kujaribu kuifanyia kazi. Mwandishi mmoja mwanamke aliye kwenye miaka ya hamsini anasema:

Ninaamini hofu ya kuwa na uhusiano wa karibu ni jambo lenye mantiki – namna ya kujilinda kulingana na mazingira inayozuia kujikuta umenasa kwa mtu asiye sahihi. Na kulingana na bahati yako, hutokomea pale unapompata mtu sahihi. Inapofikia wakati kama huu, unaacha kuhofia kuhusu maziwa yako yaliyolegea na mapaja yako yaliyokunjamana, haja yako ya kuwa na udhibiti, na hofu kwamba ataanza kupumua akiwa kitandani pale mtakapozoeana sana. Nguvu inayoachiwa huru katika mchakato huu inaweza sasa kuelekezwa katika kuomba unachohitaji, kuwazia kitu unachokitaka, na kupanga mipango thabiti ya kufaniki ndoto zako.

Wengi wetu ambao tumeshawahi kukumbwa na kiwewe cha kihisia au kimapenzi katika maisha yetu tunaweza kuwa na hofu hata kama tupo mahali salama. Hisia mbaya na za kuchanganya zinaweza kuibuka katika uhusiano wa karibu kama matokeo ya kiwewe cha hapo siku za nyuma, mara nyingine kwa kipindi chote cha maisha (tazama Sura ya 8, “Ukatili na Uonevu”). Kujadiliana na mwenzi juu ya hali hii inaweza kuwa ngumu; inaweza pia kuwa ni sehemu ya mchakato wa kupona. Namna mwenzi wako anavyochukulia hali yako inaweza kuwa ni ishara ya kiwango chake cha hisia, na ya uwezo wake wa kuweza kushughulikia masuala muhimu, kuwasiliana, na kuhusiana na hisia nzito. Kuongezeka kwa kiwango cha hisia kwa pande zote mbili juu ya kiwewe cha kimapenzi cha siku za nyuma kunaweza vilevile kuteng’eneza vikwazo vipya, pamoja na mawasilano mazuri, na ukaribu zaidi.

Mahusiano Na Wanaume (“Relationships with Men”). For more information, see:
<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

Imekuwa ikisemekana kwamba mapenzi ni ya baina ya watu wawili waliojitoa kikamilifu. Hakuna mtu, bila shaka, aliyekamilika. Lakini bado tunaweza kuukaribia ukamilifu kadiri tunavyohusiana na wale tunaowapenda. Tena ukamilifu unaweza kutafutwa hata baada ya kitu kuwa kimechukuliwa, kimevunjwa, kimedhuriwa, au kuachwa bila kufaywa. Mambo ya yaliyopita yanaumiza, ingawa yanaweza kutuletea hofu na vikwazo katika uhusiano wa karibu, yanaweza pia kutufundisha kuwa jasiri na kutufanya tuingie kwenye mahusiano tukiwa na huruma busara zaidi. Iwe tunataka kuanzisha mahusano mapya au kuboresha yale ya zamani, tunaweza kujumuisha uzoefu wetu wa zamani kwenye mahusiano ya sasa wakati tunapokuwa tunajadili mivutano kati ya hali ya kuwa huru na kujitegemea, vitendo vya kimapenzi na haja ya kubakia tumetengana.

Kitu kimoja cha uhakika kuhusu ndoa yangu ya pili ni kwamba kwa sababu nina umri mkubwa zaidi kuliko mwenzangu, na kwa sababu ya vile jinsi Rob alivyo, niko karibu naye zaidi kuliko mume wangu wa kwanza. Nina uwezo wa kumjali zaidi na kwa undani zaidi pia. Na kwenye nyakati anazokuwa hayupo, hata kwa usiku mmoja, huwa naumia sana. Si kwamba “Oh Mungu wangu, siwezi kujitunza mwenyewe”, hapana, kwa sababu nina kila kitu na ninaweza – ila ni kumkosa mtu kutoka moyoni. Ni kitu cha kushangaza lakini, kwa sababu mimi ni muungaji mkono mzuri wa harakati ya wanawake inayojulikana kama “Ajenda ya Mwanamke mwenye Uwezo wa Kipekee” inayolenga kuwafanya wanawake wenye kujitegemea kwa kila kitu.

Lakini bado wazo linanijia namna gani nitakavyoumia endapo kitu chochote kitambkumba Rob, jinsi maisha yangu yatakavyokuwa na upweke.

MAKUBALIANO, MWENZI MMOJA, NA NDOA

Wengi wetu tunaofanya mahusiano ya kudumu na mwenzi mmoja wa kiume mwishowe huamua kuolewa. Tunafanya hivi kwa sababu mbalimbali: kwa sababu tunataka kuenziwa na kuungwa mkono kwa penzi letu kati yetu na wenzi wetu; kwa sababu tunaamini kwenye ndoa kuna uhakika wa kupata mahitaji yetu na kukua kiroho pia; kwa sababu tunataka kunufaika kiafya, kuwa na haki za kumiliki mali, kunufaika kwa kupata mahali pa kuishi; kwa sababu tunataka watoto na tunataka wakulie kwenye familia inayotambuika kisheria.

Niliolewa kwa sababu nilitaka kuwa na hali ya uhakika wa kudumu; Nilitaka uhusiano unaonifunga kisheria kama ilivyo katika ndoa.

Nilikua na hofu kuwa ndoa inaweza kuniondolea uwezo wa kufanya kitu nilichokipenda – kazi. Niliolewa nikiwa na umri wa miaka 28 kwa sababu nilikutana na mwanaume aliyenifanya nijisikie kuwa utimilifu wangu ndio ulikuwa kitu muhimu zaidi kwake. Nilitaka kuolewa na rafiki yangu mkubwa, na yeye ndiye siku zote amekuwa rafiki yangu mkubwa.

Taasisi ya ndoa ina historia ndefu ya kuwakandamiza wanawake, kwa kutunyima haki zetu za kumiliki mali na kujitetea dhidi ya wenzi waonevu, na kwa kutilia mkazo majukumu yaliyozoeleka ya kila jinsia kwenye ndoa. Nusu ya ndoa zote nchini Marekani huishia kwa wanandoa kutalikiana. Lakini hata kama

tunaichukulia ndoa kama taasisi yenye mapungufu – au hata ya kigandamizaji, msingi bora wa familia, au kitu ambacho ni vigumu kukielewa, bado wengi wetu tunataka kuolewa na kuingia kwenye ndoa.

Niite nisiye na msimamo, lakini nimeshaamua kwamba naweza kuishi ndani ya mipaka ya ndoa ya kisheria na kuifurahia. Naweza “kuchagua njia rahisi” na wakati huohuo nikijaribu kujijengea mitazamo mipya juu ya maana hasa ya ndoa. Na kwa njia ndogondogo, zinazoweza kuonekana kutokuwa na umuhimu wowote nitaweza kupunguza baadhi ya mizigo ambayo ndoa – na hasa harusi – huambatana nayo. Ninaweza kukatiza katikati ya kanisa kuelekea altareni bila kusindikizwa na baba yangu; Ninaweza kukataa pete ya uchumba; Ninaweza kubaki na jina langu; Ninaweza kupendelea kuwa na “patna” badala ya “mchumba” au “mke.” Mimi na patna wangu tunaweza kuweka wazi makubaliano yetu ya sasa na ya muda mrefu kwa namna ambayo jamii na wazazi wetu wanaelewa, na kufanya karamu kubwa.

Wanawake wengi wanahisi kuwa sherehe ya harusi – iwe ya ‘kitamaduni’ au la, ni kitendo cha heshima kinachoweza kuwafanya mtu na mkewe waunganike wao wenyewe na vilevile waunganishwe na jamii kiundani zaidi.

Kwa kukubali taratibu za ndoa, ninathibitisha kuwa mimi pia ninachukulia tendo la kufunga ndoa kama mapatano matakatifu; liko juu ya mambo tunayofanya kila siku lakini kwa wakati huohuo linadhihirisha utakatifu wa maisha yetu ya kila . Ahadi ya makubaliano bila msaada wa jamii inaweza kuvunjika kirahisi. Taratibu za ndoa

kunawapa wanandoa fursa ya kudumisha uhusiano kati ya maisha binafsi ya ndoa na msaada kutoka kwenye jamii.

Baadhi ya wanawake wanaona kuwa ndoa huwapa utulivu na kuwafanya wawe na amani, na watambulike kwenye jamii. Hi inaweza kufanya uhusiano ustawi.

Naapa, mama yangu alikuwa akimwita mara kwa mara Colin kama “huyo jamaa” (kama alivyokuwa akirudiarudia kusema “Huyo jamaa atakuja kukuo a lini?”) Mara tu baada ya kunivisha pete ya uchumba, sasa akawa “Colin” – mtu aliyekamilika, na sio tena “jamaa aliyekuwa akikamua bure.” Jamaa mzuri kama Colin, inafurahisha kuwa naye kwenye familia, n.k. Bila shaka niitaka kuolewa. Harusi kubwa na zawadi za aina mbalimbali – nimekuwa nikivisubiri kwa hamu sana! Lakini ukweli ni kwamba...mpake pale Colin alipotoa ile ahadi akisema: “Nataka kukuo a” – siku zote nilikuwa sijiamini sana, na hata uaminifu wangu kwake haukuwa timilifu.

Na bado ni jambo la muhimu kujaribu kuweka pembeni shinikizo la kifamilia au kijami wakati wa kufanya uamuzi wa kuo a. Kwa kuangalia mbali, ni maisha yetu na ya wenzi wetu, tutakapokuwa pamoja, ndio ya muhimu zaidi. Linapokuja suala la kudumu, mwanamke mmoja mwenye miaka hamsini na kitu hivi mwenye watoto wawil watu wazima anasema hakuna nafasi au muda wa kutosha kuelezea undani wa ndoa na “kule unakokupeleka.”

Sio katika mtazamo wa kimapenzi, ila pale unapokuwa dhaifu na unapoo na hakuna msaada. Wakati niko katika kipindi kati ya upasuaji wa pili na wa tatu wa uti wa

mgongo, si tu kwamba sikuweza kutembea, bali pia sikuweza hata kupandisha nguo yangu ya ndani. Nakumbuka pale mume wangu alipoingia chumbani kunisaidia wakati nilipokuwa najikakamua kuharakisha kwenye korido kuelekea bafuni. Namna alivyonigusa, alivyoniangalia, na kutambua kuwa nilikuwa kwenye maumivu ambayo angeyatwaa angelikuwa na uwezo...Kuna mabadilishano fulani ambayo huyafanyi na mtu yeyote. Nje ya ndoa kuna mlango wa dharura wa kutokea ulio wazi muda wote ikiwa mambo hayaendi kama ulivyopanga. Ndani ya ndoa, kuna kutambua kuwa kuna muunganiko unaofanyika zaidi ya kimwili tu...Ni kama vile tunajijambia sehemu na muda wetu wenyewe, namna yetu wenyewe ya kuwasiliana.

Wanawake wengi hukubali kuolewa huku wakiwa na ufahamu kuwa ndoa hubakia kuwa muunganiko wa kijamii usio haki kwenye dini, na kwenye majimbo mengi, kwa sababu tu ni mahusiano ya jinsia tofauti ndio hutambuliwa na dini hizi na kwenye majimbo haya.

Nadhani hatukoana katika miaka minne ya mwanzo ya uhusiano wetu kama ishara ya kuonyesha kupinga, kwa kiasi fulani...Siku zote hatukuwa tunafurahishwa na ukweli kwamba haki hii hutolewa kwa watu kama sisi tusio na tatizo lolote kimaumbile, wakati dada na kaka zetu mashoga na wasagaji hutungiwa sheria zinazowazuia kufanya muunganiko unaotambulika kisheria. Hivyo hatukuona kuwa ni haki kwa sisi kushiriki "manufaa" haya wakati kuna kundi lingine la watu wananyimwa haki hizi.

Idadi inayoongezeka ya wachumba ambao hawakubaliani na taasisi ya ndoa wanapendelea kuishi pamoja kwa furaha chini ya makubaliano wanayowekeana wenyewe, ambayo yanaweza kujumuisha au kutojumuisha kupata watoto. Jamii pia zinategemea wachumba kama hawa kuwiana, kusaidiana na kudumu kwa muda mrefu.

Siwezi kufikiria maisha yangu bila patna wangu – ananihifadhi, ananisaidia na ananifurahisha. Tumeshibana hasa, na tumekuwa hivi kwa muda wa miaka 11. Lakini ndoa inaonekana kutokuwa na umuhimu katika aina ya maisha tunayoshirikishana – kwa kifupi, haina uhusiano wowote na mapenzi yetu wala makubaliano tuliyowekeana. Kwa kiasi kikubwa marafiki na familia wamekuwa waelewa na wenye kuunga sana mkono uamuzi wetu wa kutokuona. Mwaka jana, tulitumia nafasi ya kuadhimisha miaka 10 ya kuwa pamoja kuwafanyia marafiki na familia zetu tafrija kubwa, ili nao washerehekee makubaliano yetu pamoja nasi.

Wakati wengi wetu tunategemea uhusiano na mapatna wetu utadumu maisha, ukweli usiopendeza ni kwamba idadi kubwa ya mahusiano haya huishia kwa kutengana au kutalikiana. Mchapishaji mmoja mwenye miaka thelathini na tatu anaelezea ndoa yake asiyokuwa ameitarajia – na mbaya zaidi kutalikiana kusikokuwa kumetarajiwa.

Sikutegemea kabisa kuolewa. Kwanza sikutaka kuichukulia ndoa kama lengo. Pale nilipokutana na mwanamume niliyeishia kuolewa naye, nilishtukizwa sana na hali yangu a kutaka kuolewa na kuishi naye. Ulikuwa ni uhusiano wenye nguvu na ulikua

haraka sana, na tulitaka kuwatangazia watu juu ya makubaliano yetu ya kuishi pamoja (kwa kiasi fulani kutoa ujumbe kwa marafiki na familia pia kwamba ilikuwa si utani, licha ya uharakishwaji wa jambo hilo) na, nakubali, ili kunufaika na faida za “kukubalika” kwa uhusiano ambazo huambatana na ndoa (na manufaa mengine ya uhusiano baina ya watu wa jinsia tofauti). Kwa kifupi, miaka minne baadaye, alikuwa na uhusiano na mwanamke mwingine nje, na muda si mrefu ikawa wazi kuwa uhusiano wetu usingeweza kuokolewa tena (na bila shaka ulikuwa na dosari kibao ambaz nilikuwa nakataa kuzikubali).

Wakati kuvunjika kwa uhusiano, hasa ule uliotoa ahadi ya makubaliano ya kudumu maisha, kunaweza kuambatana na uchungu mwingi, kunaweza pia kumpelekea mtu kujitambua na kujua ni vitu gani hasa anahitaji. Mchapishaji huyu wa miaka thelathini na moja anaendelea kuelezea:

Kipindi cha kutalikiana na kutengana kwetu kilikuwa kigumu na cha kuumiza sana. Zaidi ya mwaka mmoja umepita sasa, lakini bado nahisi athari zake, lakini baada ya kujitahidi kusahau (kwa msaada wa marafiki na familia, na mtaalam wa mmoja mzuri sana wa matibabu), sasa ninaelewa zaidi ni kitu gani ninataka na ninahitaji kutoka kwa mwenzi nitakaye kuwa naye, azimio jipya nililojiwekea la kutokubali tena kupofushwa na mawazo yale ya awali, na uthibitisho wa kile nilichokuwa nakifahamu siku zote: kwamba nina furaha kubwa sana nikiwa peke yangu bila mwenzi.

Wakati kuna baadhi ya watu wanachukulia mahusiano ya kudumu na mwenzi mmoja kama kitu kinachofaa zaidi, wengi wanatafuta mahusiano huru – kuwa na

mahusiano ya kimahaba na watu wawili au zaidi kwa wakati mmoja – ama kwa kipindi cha muda mfupi au kwa maisha yote (kama ilivyo kwa ndoa huru, ambapo wenzi hukubaliana kuwa kila mtu anaweza kuwa na mahusiano ya kimapenzi na watu wengine). Wanawake wengine hupendelea kuwa na wapenzi wengi, ambapo tunakuwa na mahusiano ya kudumu na mtu zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja.

Kwangu mimi kuwa na wapenzi wengi ni suala la kuwa na mahusiano mengi ya karibu ambayo hayatofautisiki yangu; na wakati mwingie ninaweza kuwa na uhusiano imara wa kudumu na mtu ambao haujumuishi kufanya mapenzi. Kwa sasa nina mapatna watatu wazuri sana, ambao wote ninawapenda sana. Nimekuwa na wawili kati yao kwa kama miaka minne hivi, na uhusiano wangu na huyu mwingine una miezi michache. Wanatofautiana sana kiasi kwamba kila mmoja anaweza kuniridhisha kwa namna ambayo wengine hawawezi. Hiki ndio kitu ninachokipenda juu ya kuwa na wapenzi wengi. Ninaweza kuangalia vipindi vya kuburudisha vya televisheni na patna mmoja, na kucheza na kompyuta na patna mwingine. Mapenzi sio kitu chenye mipaka – naamini kadiri mnavyoshirikishana, ndivyo yanavyozidi kustawi.

Kwa baadhi yetu, kuwa na uhusiano na mwenzi mmoja sio jambo la lazima, ila ni kitu tunachojifunza na kukipokea kwenye jamii kama njia ya kuonyesha uaminifu wetu kwa wenzi wetu.

Labda niwe muwazi tu kwamba suala la kuwa na mwenzi mmoja halijawahi kuwa kitu cha muhimu sana kwangu. Nadhani hii imesababishwa na Nancy Reagan!

Nilikuwa msichana mdogo wakati wa miaka ya Reagan, wakati ndio naanza kujaribisha hisia zangu za kimapenzi), na mtazamo wa kipindi hicho ulikuwa “Sema Hapana kwa Chochote.” Lakini wengi wetu tulijiambia “Hebu Ngoja Tujaribishe.” Hivyo, kulikuwa na majaribio mengi tu yakiendelea kwa upande wangu na kwa wasichana wenye umri kama wangu ambayo nadhani yalikuwa na manufaa sana, na kutufanya tufumbuke zaidi kiakili. Niko kwenye uhusiano na mwenzi mmoja kwa miaka kumi na moja sasa, kwa sababu mume wangu ananitaka niwe hivi ili niweze kuwa kwenye uhusiano na yeye – huo ndio msimamo wake. Ilikuwa ngumu mwanzoni lakini kwa sasa, hamna shida.

Ikiwa unafikiria kuingia kwenye ndoa au kuweka ahadi kwa makubaliano ya muda mrefu, na hauna uhakika kama ni sahihi kwako kufanya hivi, bila shaka kuzungumza na mwenzi wako ni wazo zuri. Zaidi ya hapo, marafiki au wenzako ambao nao pia wameshakuwa na mawazo ya kuingia kwenye ndoa wanaweza kukupatia mitazamo mipya. Ikiwa upo kwenye uhusiano wenye makubaliano ya ahadi ya kuwa pamoja kwa muda mrefu, na mnajadili juu ya kufunga ndoa, kupata nasaha kabla ya ndoa linaweza kuwa jambo lenye manufaa (na ni lazima kwa baadhi ya mashirika ya dini kupata ushauri huu). Pia kuna mashirika ya kidini yanayotoa dondoo na ushauri wa kisheria, na utetezi wa kisheria kwa wenzi ambao hawataki kuoana lakini wana shauku ya kufanya uhusiano wao kuwa halali kisheria na kijamii.

KUFANYA MAMBO YAENDE SAWA: UWEZO WA PAMOJA

Mahusiano Na Wanaume (“Relationships with Men”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

Kwenye uhusiano wowote, matatizo hutokea bila kujalisha kwa kiasi gani kila mmoja yu “sahihi” kwa mwenzake, kwa kiasi gani tumefanya juhudi kuujenga uhusiano huo, na hata kwa kiasi gani tuna mshikamano na tunajiona imara pamoja. Inaweza kuogopesha kidogo kukabiliana na jambo linalotutatiza na linaloumiza. Tunataka kuamini kuwa tumechagua patna mzuri na maamuzi tuliyochukua ni ya busara. Kuwa na ufahamu kuhusu mambo ambayo tumekuwa tukiogopa kuyakabili, au kuruhusu migongano, kunaweza kumaanisha kuwa tumefanya kosa kubwa, na kuwa itachukua muda mrefu sana kushughulikia suala hili, au kuwa ni wakati wa kusahau yaliyotokea na kuendelea na maisha yetu.

Wakati uwezo binafsi wa mtu ni msingi muhimu kwa uhusiano mzuri, kutengeneza uwiano mzuri kiuwezo ni suala kuzingatia pia. Kuwa na uwezo wa pamoja kwenye uhusiano mzuri kunahitaji, na hupelekea kujiendeleza kila mara – na kunatoa nafasi isiyo na mwisho ya kuuimarisha uhusiano. Kuyakabili matatizo na kuchukua hatua za ili kufanya mabadiliko pia kunaweza kuwa kitu cha kuogopesha, lakini kwa kujiamini na msaada kutoka kwenye jamii zetu, na kwa uaminifu unaotokana na kushirikishana sana, wanawake na wanaume wanaweza kutambua njia mpya za kuwa pamoja ambazo zinawafanya wawe huru zaidi.

Kufanya mahusiano yafanikiwe kunahitaji mbinu. Kwa bahati nzuri, tunaweza kujifunza mbinu hizi. Zifuatazo ni baadhi ya mbinu za msingi ambazo wanawake na wanaume wengi wamejaribu kujifunza ili kuwasaidia kufanya mambo yaende vizuri kwenye mahusiano.

KUKUZA MAWASILIANO MAZURI

Tabia ya kuepuka kulikabili tatizo mara nyingi husababisha mahusiano kudorora na kukuacha na hasira badala ya kukuacha na amani au kuboresha mambo. *Mgogoro unaweza kuwa sehemu ya mchakato bunifu wa kutatua matatizo. Tunaweza kuanza kwa kutambua vipengele vya mgogoro wetu ambavyo tumerithi kutoka kwenye jamii na familia zetu, na kuepuka mtego unaowashinda wengi wa kulaumiana (au kujilaumu wenyewe) kwa kila kitu ambacho hakiendi sawa.*

KUHOJI MATARAJIO YETU

Kupitia upya fikra zetu na kujaribu kung'amua mawazo ya wapenzi wetu kunaweza kutusaidia kufanya majadiliano kwa njia ya ubunifu. Kujaribu kuachana na majukumu yetu ya zamani, hasa yale yanayotokana na mambo yanayochukuliwa kama desturi kwenye jamii, na kujaribu kuwa kwenye uhusiano bila mawazo au matarajio kunaweza pia kutusaidia kutambua mfumo wetu wenyewe wa kuhusiana na wanaume. Kadiri tutakavyoweza kufanya hivi mapema, ndivyo uhusiano wetu utakavyokuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kustawi. Watu wote huingia kwenye mahusiano wakiwa na matarajio fulani. Swali ni kwamba, kwa kiasi gani tuko tayari kuyabadilisha ili tuweze kuwa na wenzi wetu?

KUTENGA MUDA WA KUWA PAMOJA

Mahusiano Na Wanaume (“Relationships with Men”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

Mambo mengi sana yanachuana kupata umakini wetu: kazi, marafiki, watoto, shughuli zetu mbalimbali na kazi ndogo ndogo za kila siku. Penzi jipya huyafanya haya yote yasionekane, lakini baada ya muda si mrefu, linaweza kujikuta katikati ya misukosuko ya mahitaji ya familia zetu, majukumu yetu ya kikazi, marafiki zetu. Mahusiano ya karibu ya kimapenzi hutufanya turidhike na hutuachia kumbukumbu za kudumu maishani mwetu, lakini mara nyingine yanahitaji umakini wetu wote. Hii inaweza kumaanisha kuwa na siku maalumu mara moja kwa wiki, au kutenga muda wa kuzungumzia yaliyojiri kwa siku nzima, kazini na nyumbani; inaweza kumaanisha, mara kwa mara, kukaa macho mpaka usiku wa manane kujaribu kutatua mgogoro na/au kupeana mahaba motomoto. Kwa wengi wetu, hii humaanisha kujaribu kuwa waangalifu, wachangamfu, na kuwa pamoja na wenzi wetu kwa muda wote.

KUFURAHIA KUWA MBALIMBALI

Inaweza kuonekana jambo la kawaida kwa wengi wetu kwenda likizo kivyetu au kuwa na marafiki wetu wenyewe tofauti na wenzi wetu. Wengine wanaweza kuchukulia hili kama ishara kuwa kuna kitu hakiko sawa. Kuna wakati mmoja wa wapendanao anaweza kuogopeshwa pale anapokuwa hashirikishwi kwenye maisha ya mwenzi wake kwa namna moja au nyingine. Lakini kuwa na maisha yetu tofauti – iwe vitabu mbalimbali vya hundi, kwenda likizo kivyetu, marafiki tofauti, vyumba mbalimbali, au kutokuharakisha kuishi pamoja – si lazima kutishie uhusiano wetu. Kunaweza kukuza na kuongeza uhai kwa kila jambo linaloendelea kutuzunguka.

KUONGEZA MARAFIKI NA KUPANUA MAHUSIANO NA JAMII KWA UJUMLA

Wakati mwingine wenzi hujitenga na maisha yanayowazunguka. Tunaweza kuyapa umuhimu mdogo mahusiano mengine na kuyaacha yafe. Lakini ni kitu kisichowezezana kutegemea kuwa mtu mmoja anataweza kutimiza mahitaji yatu yote. Mahusiano yetu ya kirafiki na jamii zinazotuzunguka – ya kidini, kisania, kisiasa, majirani, n.k. – ni muhimu sana kwa afya yetu kihisia, furaha na ukuaji wetu pia. Zaidi ya hapo, kwa kupanua wigo wa watu wa karibu, tunapunguza baadhi ya mashinikizo yaliyopo kwenye mahusiano yetu muhimu, na kwa kipindi ambacho mambo ni magumu, watu wengine wanaweza kutupa msaada. Hii inajumuisha kuwa na marafiki wa kiume pamoja na wa kike.

KUFAHAMU WAKATI WA KUONDOKA

Kama utaishia kuonyesha fadhila kwa mwenzi wako ili tu kuzuia ugomvi usitokee, badala ya kuwa na matumaini kwamba ni heri kujaribu kutatua matatizo; kama uhusiano wenu umejikita kwenye kupa mambo yanayotakiwa kufanywa, udanganyifu na kutotumia kwa pamoja vitu mbalimbali; kama una sifa ya kutokuwa na nafasi ya mabadiliko na kukua; au kama tu haionekani kwamba maisha yako ni bora zaidi ukiwa ndani ya uhusiano kuliko kama ambavyo yangekuwa nje ya uhusiano huo, basi ni muda muafaka wa kuanza kufikiria kusitisha uhusiano huu. Si lazima ufanye hivi peke yako. Marafiki wanaweza kuwa chanzo kizuri kabisa cha

Mahusiano Na Wanaume (“Relationships with Men”). For more information, see:
<http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

msaada na mawazo. Tiba ya mtu mmoja mmoja au kundi inaweza kusaidia pia. Pia, kuna vitabu vizuri juu ya jambo hili (tazama “Msaada”). Kama ilivyo muhimu kutumia juhudi kubwa katika kujenga uhusiano, ni muhimu pia kujitoa kwenye uhusiano mapema kabla haujatudhuru. Ikiwa una wasiwasi kuwa uhusiano wako unaweza kuwa wa kionevu, tazama Sura ya 8, “Ukatili na Uonevu.”)

KUPATA MSAADA

Kama hatutaki kuondoka, au kama tunajitahidi kutambua ikiwa ni muda muafaka wa kufanya hivyo, tunaweza kuhitaji msaada. Kuna wakati matatizo hukinzana na mabadiliko, na inaweza kuonekana kama vile haitusaidii chochote tunapozungumza na wanafamilia na marafiki. Pale tunapona kuwa tumekuwa tukihangaika na jambo moja kila wakati na bado hakuna maendeleo yoyote, tunaweza kuzidiwa kabisa na kuhisi kukwama kwenye ruwaza tusizoweza kuzibadilisha wenyewe. Na hapo ndipo tunaweza kutafuta msaada wa tiba, ama peke yetu au pamoja na wenzi wetu.

Mimi na mpenzi wangu tumekulia katika nyumba zilizokuwa na vitendo vya uonevu. Matokeo yake, hatukuwa na mfano wa kuiga wa ugomvi wa kistaarabu. Malumbano yetu yangeweza kuwa makubwa sana – na kila baada ya hapo kila mmoja alikuwa ametumia udhaifu wa mwenzake, na kuumizana vibaya sana kiasi kwamba ilikuwa ni ngumu sana kuzungumza tena kistaarabu...Wote tukiwa tunatokea kwenye familia za Kusini mwa bara la Asia, mimi na mpenzi wangu tuliamua kumtafuta mshauri

Mahusiano Na Wanaume (“Relationships with Men”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

nasaha anayetokea Kusini mwa bara la Asia pia – pengine labda tungempata mtu ambaye tusingekuwa na haja ya kumwelezea masuala yanayohusu utamaduni, na ambaye angeweza kuyachukulia matatizo yetu, ambayo yalikuwa yanagusa mpaka familia zetu, kwa mtazamo wa Kiasia Kusini. [Mshauri wetu] alikuwa mzuri sana. Alitulia moyo wa kuwekeana “mipaka” na kuahidi kutoivuka kamwe. Pale tulipoona mmoja kati yetu anasogelea mpaka binafsi wa mwenzake, angeweza kumpa tahadhari, na kumwomba asifike huko. Tulijifunza pia “kufanya marudio” ya malumbano yetu baadaye, na kufikiria kibunifu ni hatua gani kila mtu angeweza kuchukua ikiwa mwenzake angefanya kitu tofauti na alivyofanya. Vitendo kama hivi vimetusaidia kuelewa ni aina gani ya maisha kila mmoja anatokea.

Wakati tunaweza kutumia tiba kusaidia kuboresha mawasiliano katika masuala yanayotuumiza, ni muhimu sana kuchagua mtaalaam sahihi wa tiba. Ni muhimu kutafuta mtaalaam ambaye uelewa wake wa afya na “hali ya kawaida” umejikita kwenye mtazamo kwamba wanawake wana machaguo ya kila aina, na sio kwenye mtazamo finyu, kama vile fikra ya kuwa kazi pekee ya wanawake ni “kuwahudumia” wanaume na kutunza watoto. (Kwa maelezo zaidi, tazama Sura ya 6, “Hisia Nzuri.”

WASIWASI WA KIBUNIFU

Ingawa inaweza kuonekana kitu chenye kuhitilafiana kutaka ukaribu na wenzi wetu na wakati huohuo kutafuta uwezo binafsi, na mahusiano mengine ya kirafiki,

Mahusiano Na Wanaume (“Relationships with Men”). For more information, see: <http://www.ourbodiesourselves.org/tanzania>.

vipengele hivi mbalimbali vya maisha yetu huweza na mara nyingi hustawishana. Vinaweza pia kuleta uwiano ambao huchochea ukuaji na huongeza afya kimwili, kiakili na kiroho. Mwanamke mmoja mtu mzima wa miaka sitini na nne, ambaye mwenyewe amekuwa kwenye ndoa kwa muda mrefu na anafurahia kuwa hivyo, anaepuka neno “ndoa” huku akisema kuwa anaamini kwa moyo wote makubaliano ya ahadi ya kuwa pamoja kuwa ndio mazingira ambayo ukaribu unaweza hasa kukua.” Anaongezea:

Bila shaka, ukaribu wa kimwili unaweza kutokea haraka na unaweza kuwa dalili ya ukaribu katika nyanja zote. Ukaribu wa kweli (yaani, ukaribu unaofika mpaka kwenye kiini cha moyo wako) unahitaji muda kuupata, na kwangu mimi na mume wangu zaidi ya miaka 40, ya shughuli nzito, na bila shaka kusameheana. Kuweka uwiano sahihi kati matakwa yetu binafsi na yale ya pamoja katika uhusiano aghalabu huwa ni suala gumu kulifanikisha, lakini kukiwa na kujitoa kwa ajili ya uhusiano, wasiwasi unaweza kuwa – na, ili uishe, unatakiwa uwe – wasiwasi wa kibunifu.

Pengine sisi ni wanandoa wenye sifa ya kipekee kwa sababu ilimbidi mume wangu afanye jitihada ya kuushinda ukaidi wa kutotaka “kuwa muwazi” – ambako kungemfanya awe dhaifu mbele yangu – na ilinibidi kuwa mstahimilivu katika kuhamasisha uwazi wa namna hiyo kwa pande zote mbili huku nikiheshimu anakotoka. Ni hamu yetu ya kuwa na uhusiano unaokua ndio imekuwa ikitufanya tuendeleo kujaribu (mara nyingine hatua mbili mbele, moja nyuma). Lakini cha

kushangaza ni kwamba, katika suala hili zima hakuna hata mmoja wetu anayejiona kudhoofishwa, ila kunufaika. Katika ila hatua tunayopiga katika kuelewana, ukaribu wetu unazidi kukua.